



## HAKIKISHA KUWA UNA TAAUSIKU

Huko Vermont, ajali nyingi zinazohusisha watu kutembea, kuendesha baiskeli na kubingirika hutokea katika hali ambapo hakuna mwangaza, kama vile kwenye barabara za mashambani usiku na katika majira ya majani kupukutika na majira ya baridi.

Ikiwa unatembea kwa miguu au unaendesha baiskeli, hakikisha kuwa unaweza kuonekana na kuwa uko salama wakati wa usiku kwa **kuvaa viakisi** na **kubeba taa** kila wakati. Madereva pia wanapaswa kuwa waangalifu na kuwa macho zaidi ili waone watembea kwa miguu wanapoendesha gari usiku.

### **JINSI YA KUTUMIA VIAKISI:**

Viakisi vinapaswa kuonekana kutoka mbele na nyuma. Viakisi vinapaswa kuning'inia. Madereva huona kitu au mtu anayesogea zaidi kuliko jinsi wanaovyooona kitu kinachoakiksi kisichosogea.

Ambatanisha viakisi kwenye:

- Mabegi ya mgogoni
- Mifuko
- Zipu
- Vifaa vya kusaidia kutembea
- Viti vya magurudumu
- Kanda za kufungia au kuongoza mbwa
- Ni vizuri kuwa na viakisi vingi, kadri iwezakanavyo!

**Mtu aliyevaa kiakisi anaweza **kuonekana mara 3 zaidi** kuliko mtu aliyevaa mavazi meusi.**

# Vidokezo vya Usalama Usiku kwa Watembea kwa miguu, Waendesha baiskeli na Madereva

## KWA WATEMBEA KWA MIGUU NA WAENDESHA BAIKELI:

- Hakikisha kuwa madereva wanaweza kukuona kwa kuvaa mavazi mepesi na angavu, au bora zaidi, beba tochi/taa za baiskeli na uvae nguo za kuakisi.
- Waendesha baiskeli wanatakiwa na sheria kutumia mwanga mwekundu unaomulika au thabiti AU angalau inchi 20 za mraba za nyenzo inayoakisi iliyowekwa upande wa nyuma.
- Vuka barabara katika maeneo yenye mwanga mzuri ambapo unaweza kuona trafiki vizuri zaidi.
- Tumia vijia vya watembea kwa miguu inapowezekana.
- Katika kituo cha basi: vuka barabara ukiwa nyuma ya basi au kwenye barabara zilizochorwa za watembea kwa miguu.
- Kuwa mwangalifu ili uone magari, baiskeli na magari mengine - kwa sababu huenda waendeshaji hawakutazami.

## UNAPOENDESHA GARI:

- Tii sheria za viwango vya mwendo. Mtembea kwa miguu aliyegongwa na gari linaloendeshwa kwa mwendo wa maili 40 kwa saa ana uwezekano wa asilimia 85% wa kuuawa. Ikiwa gari linaendeshwa kwa mwendo wa maili 20 kwa saa, hatari ya kuuawa inapungua kwa asilimia 5%.
- Epuka kuendesha gari ukiwa umevutwa mawazo, kuendesha kwa fujo na kuendesha gari ukiwa umekunywa pombe au umetumia dawa za kulevya.
- Hakikisha kuwa umesimamisha gari kabisa kwenye ishara za kusimamisha gari na taa nyekundu.
- Kaa macho, tazama baiskeli na watembea kwa miguu kila wakati na uruhusu watu wengine watumie barabara.

Maelezo zaidi yanapatikana kwenye: [SafeStreets.Vermont.Gov](https://www.SafeStreets.Vermont.Gov)